

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS - TAMISEMI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU

UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO  
CHA KWANZA MWAKA 2020 TANZANIA BARA

Ndugu Wananchi,

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imekamilisha zoezi la uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2020 ambapo jumla ya wanafunzi **759,737** walifaulu sawa na asilimia **81.3** ya waliofanya mtihani, wakiwemo wavulana **363,999** sawa na asilimia **47.9** na wasichana **395,738** sawa na asilimia **52.08**. Kati ya waliofaulu wamo wanafunzi wenye Ulemavu **1,461** sawa na asilimia **0.19** wakiwemo wavulana **777** na wasichana **684**.

Ndugu Wananchi,

Baada ya zoezi la uchaguzi kukamilika, wanafunzi **701,038** sawa na asilimia **92.27** wakiwemo wavulana **335,513** sawa na asilimia **47.86** na wasichana **365,525** sawa na asilimia **52.14** wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2020.

Kati ya wanafunzi waliochaguliwa, wanafunzi **3,145** sawa na asilimia **0.41** ya waliofaulu wamechaguliwa kuijunga na shule za bweni, kwa mchanganuo ufuatao wanafunzi **970** watajiunga na shule za Wanafunzi wenyewe Ufaulu Mzuri zaidi; wanafunzi **1095** watajiunga na shule za Ufundi na wanafunzi **1,080** watajiunga na shule za bweni kawaida. Aidha, wanafunzi **697,893** sawa na asilimia **99.59** wakiwemo wavulana **361,866** na wasichana **395,692**) wamechaguliwa kuijunga na shule za sekondari za kutwa katika kata mbalimbali nchini.

### **Ndugu wananchi,**

Jumla ya Mikoa 13 ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Kilimanjaro, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Singida na Tabora. imeweza kuwachagua wanafunzi wote waliofaulu kuijunga na Kidato cha kwanza mwaka 2019 katika shule za Sekondari za Serikali.

Aidha, jumla ya wanafunzi **58,699** sawa na asilimia **7.73** wakiwemo wavulana **28,567** sawa na asilimia **48.53** na wasichana **30,132** sawa na asilimia **51.33** ya waliofaulu, hawakupata nafasi ya kuchaguliwa kutokana na uhaba wa vyumba vyatya madarasa. Mikoa yenye uhaba wa vyumba vyatya madarasa na idadi ya wanafunzi waliobaki ni Arusha (4,739), Dar es salaam (5,808), Iringa (3,480), Kigoma (12,092), Lindi (1,695), Manyara (728),

Mara (9,493), Mbeya (2,716), Pwani (2,918), Rukwa (686), Simiyu (6,616), Songwe (4,684) na Tanga (3,044). Wanafunzi hawa waliobaki watajiunga na kidato cha kwanza baada ya vyumba vyaa madarasa kukamilika.

**Ndugu wananchi,**

Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wanafunzi wote waliochaguliwa kuijiunga Kidato cha Kwanza katika shule za Sekondari. Pia nawashukuru Walimu, Walimu Wakuu, Kamati za Shule, Maafisaelimu Kata, Wilaya na wa Mikoa pamoja na Viongozi wote wa Halmashauri na Mikoa na Wadau wa Elimu Nchini kwa kutoa ushirikiano katika kusimamia uendeshaji na utoaji wa Elimu bora Nchini. Napenda kuwaasa wanafunzi wote waliochaguliwa kutumia fursa hii vizuri katika kujifunza. Aidha, ninawaagiza walimu na watendaji wa elimu katika ngazi zote kuongeza bidii katika usimamiaji na ufuatiliaji wa utoaji wa elimu ili kuboresha hali ya elimu Nchini.

**Ndugu wananchi,**

Natoa wito kwa Halmashauri wakishirikiana na wadau wote wa elimu kukamilisha majengo na kuandaa mazingira ya kuwapokea wanafunzi wote waliochaguliwa kuanza Kidato cha Kwanza mwezi Januari mwaka **2020** bila vikwazo vyaa aina yoyote

vikiwemo vya michango ili kutekeleza sera ya utoaji wa Elimumsingi bila malipo. Ninawahimiza, wazazi, walezi na jamii kushirikiana na uongozi wa Wilaya, Halmashauri na Shule, kuhakikisha kwamba wanafunzi wote waliochaguliwa wanaandikishwa, wanahudhuria na kubakia shulenii hadi watakapohitimu elimu ya Sekondari.


**Ndugu wananchi,**

Ninawaagiza Wakuu wa Mikoa na Wakuu Wilaya kusimamia mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji shulenii ili kubaini changamoto mbalimbali na hatimaye ziweze kutatuliwa kwa haraka.

Aidha, ninaagiza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya zilizobakiza wanafunzi kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ifikapo tarehe 29/02/2020 na Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri husika wasimamie utekelezaji wa agizo hili ili kuhakikisha wanafunzi wote waliobaki wanajiunga na Kidato cha Kwanza ifikapo tarehe 02/03/2020.

**AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA**

  
**Selemani S.Jafo (Mb)**

5 Disemba, 2019

**Waziri wa Nchi (T)**